# Haki na Ulinzi Dhidi ya Bili za Kushangaza za Matibabu

**Unapopata huduma za dharura au unapotibiwa na mtoa huduma asiye kwenye mtandao wetu hospitalini mwetu au katika kituo cha kutwa cha upasuaji, umelindwa dhidi ya bili za kushangaza (surprise billing) au malipo ya ziada (balance billing).**

**Nini maana ya "malipo ya ziada" (wakati mwingine yanafahamika kama "bili za kushangaza")?**
Unapomwona daktari au mtoa huduma mwingine wa afya, unaweza kulipia gharama fulani mwenyewe, kama vile malipo ya kugawana, bima ya kugawana na/au tozo fulani. Unaweza kulipia gharama nyingine au kulipia bili yote iwapo utamwona mtoa huduma au kutembelea kituo cha huduma ya afya ambacho hakipo kwenye mtandao wa mpango wako wa afya.
Kauli ya "Nje ya mtandao" hufafanua watoa huduma na vituo ambavyo havijaingia katika mkataba na mpango wako wa afya. Watoa huduma walio nje ya mtandao wanaweza kuruhusiwa kukutoza tofauti kati ya kiasi kilichokubaliwa na mpango wako na kiasi kamili cha huduma. Hii inafahamika kama "malipo ya ziada." Kuna uwezekano kuwa kiasi hiki kitazidi gharama za ndani ya mtandao kwa huduma sawa na huenda hakitahesabiwa kwenye kikomo chako cha kila mwaka cha bili za kujilipia.
"Bili za kushangaza" ni bili zisizotarajiwa. Hali hii inaweza kufanyika wakati huwezi kudhibiti wanaohusika katika huduma yako—kama vile wakati una dharura au wakati unapanga kutembelea kituo kilicho ndani ya mtandao lakini unatibiwa bila kutarajia na mtoa huduma aliye nje ya mtandao.

**Unalindwa dhidi ya malipo ya ziada kwa:**

**Huduma za dharura**
Iwapo una hali ya dharura ya matibabu na upate huduma za dharura kutoka kwa mtoa huduma au kituo kilicho nje ya mtandao wetu, kiasi cha juu zaidi ambacho mtoa huduma au kituo kitakutoza ni kiasi cha kugawana gharama katika mpango wako (kama vile malipo ya kugawana na bima ya kugawana). Huwezi kutozwa malipo ya ziada ya huduma hizi za dharura. Hii ni pamoja na huduma unazoweza kupata baada ya kupata nafuu kidogo, isipokuwa uwe umeandika idhini na uondoe ulinzi wako dhidi ya malipo ya ziada kwa huduma hizi za baada ya kupata nafuu kidogo.

**Huduma fulani katika hospitali za ndani ya mtandao au kituo cha kutwa cha upasuaji**
Unapopokea huduma kutoka kwa hospitali iliyo kwenye mtandao wetu au kituo cha kutwa cha upasuaji, watoa huduma fulani wanaweza kuwa nje ya mtandao wetu. Katika hali hizi, kiasi cha juu ambacho watoa huduma hao wanaweza kukutoza ni gharama za kugawana za ndani ya mpango wako. Hali hii inatumika kwa dawa za dharura, nusukaputi, patholojia, rediolojia, maabara, neanatolojia, msaidizi wa mpasuaji, mhudumu wa wagonjwa na daktari wa wagonjwa mahututi. Watoa huduma hawa hawawezi kukutoza malipo ya ziada na hawawezi kukuuliza uonde ulinzi wako dhidi ya malipo ya ziada.

Ukipokea huduma nyingine katika vituo hivi vya ndani ya mtandao wetu, watoa huduma wa nje ya mtandao wetu hawawezi kukutoza malipo ya ziada, isipokuwa uandike dhini ya kuondoa ulinzi dhidi ya malipo ya ziada.

**Hutawahi kushurutishwa kuondoa ulinzi wako dhidi ya malipo ya ziada. Pia, hutashurutishwa kupata huduma za nje ya mtandao. Unaweza kuchagua mtoa huduma au kituo kilicho katika mtandao wa mpango wako.**

**Sheria ya Jimbo la Michigan kwa Wagonjwa Wanaotumia Mipango ya Afa Inayodhibitiwa na Jimbo**
Sheria ya Michigan imeweka ulinzi kwa wagonjwa wanaotumia mipango ya afya inayodhibitiwa na jimbo.
Kwa mfano, watoa huduma walio nje ya mtandao wetu wanaohudumia wagonjwa wasio katika hali ya dharura, wanapaswa kufanya ufumbuzi fulani kwa wagonjwa kama ifuatavyo:

- Kuwa huenda bima yako ya afya isilipie huduma zote zitakazotolewa na mtoa huduma wa nje ya mtandao wako;
- Kukadiria kwa nia nzuri gharama za huduma zitakazotolewa;
- Kuwa unaweza kuomba huduma zitolewe na mtoa huduma aliye ndani ya mtandao.

**Wakati malipo ya ziada hayaruhusiwi, umelindwa pia dhidi ya hali zifuatazo:**

- Una wajibu wa kulipia mgawo wako wa gharama (kama vile malipo ya kugawana, bima ya kugawana, na matozo ambayo ungelipa iwapo mtoa huduma au kituo kingekuwa ndani ya mtandao). Mpango wako wa afya utawalipa watoa huduma na vituo vya nje ya mtandao moja kwa moja.
- Kwa jumla, ni lazima mpango wako wa afya:
  - Ulipie huduma za dharura bila kukutaka upate idhini ya mapema ya huduma (idhini ya mapema).
  - Ulipie huduma za dharura zinazotolewa na watoa huduma nje ya mtandao.
  - Uzingatie kiasi unachodaiwa na mtoa huduma au kituo (kugawana gharama) kulingana na kiasi ambacho ingelipa mtoa huduma au kituo kilicho ndani ya mtandao na uonyeshe kiasi hicho katika ufafanuzi wa manufaa yako.
  - Uhesabu kiasi chochote unacholipia huduma za dharura au huduma zinazotolewa nje ya mtandao kwenye kikomo chako cha matozo na kiasi unacholipa mwenyewe.

Iwapo unaamini kuwa umetozwa kimakosa na unalindwa na mpango wa afya unaodhibitiwa na jimbo, unaweza kuwasiliana na Idara ya Michigan ya Bima na Huduma za Kifedha (DIFS) kupitia nambari **877.999.6442** au utembelee tovuti ya DIFS ili uwasilishe malalamiko. Iwapo unalindwa na bima ya kibiashara na unaamini kuwa umetozwa kimakosa, unaweza kuwasiliana na kituo cha usaidizi cha No Surprises kupitia nambari **800.985.3059**.

Tembelea: **cms.gov/nosurprises/Ending-Surprise-Medical-Bills** ili upate maelezo zaidi kuhusu haki zako chini ya sheria ya serikali.

Tembelea: **michigan.gov/difs** na ubofye 'Surprise Medical Billing' ili upate maelezo zaidi kuhusu haki zako chini ya sheria ya Michigan.

Ili upate orodha kamili, tafadhali omba brosha kutoka kwa mtoa huduma wako wa afya au utembelee **corewellhealth.org/policies**

Corewell Health © 10.2023